

**SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR
MAHKAMA**

SIMU: 024-2230182
FAX: 024-2232720
S.L.P: 160
e-mail: registrar@judiciaryzanzibar.go.tz



OFISI YA MRAJIS
214 BARABARA YA TUNGUU
70491 KUSINI UNGUJA
ZANZIBAR

TANGAZO

Mahkama ya Zanzibar inawakaribisha wale wote wenye sifa za kuomba uwakili na uvakili, wawasilishe maombi yao kupitia mfumo ***advocates.judiciaryzanzibar.go.tz*** si zaidi ya tarehe 10/09/2023. Udahili kwa waombaji wenye sifa utafanyika tarehe 02/10/2023.

Sifa zinazohitajika kwa waombaji wa uwakili:

1. Awe amehitimu shahada ya sheria katika chuo kikuu kinachotambuliwa na Serikali;
2. Kwa aliyemaliza shahada ya sheria kuanzia 2018 na kuendelea, anatakiwa pia awe amehitimu Stashahada ya Uzamili ya masuala ya sheria kutoka Skuli ya Sheria ya Zanzibar au chuo kingine kinachotambuliwa na Baraza la Mawakili;
3. Kwa wakili kutoka Tanzania Bara, Kenya, Uganda, Rwanda, Burundi, na nchi nyengine za Jumuiya ya Madola, awe amefanya uwakili kwa kipindi kisichopungua miaka mitano mfululizo.

Viambatanisho katika maombi ya uwakili:

1. Nakala ya cheti cha shahada ya sheria,
2. Nakala ya matokeo ya kitaaluma (Transcript),
3. Nakala ya cheti cha Stashahada ya Uzamili ya masuala ya sheria,
4. Nakala ya vyeti vya elimu ya sekondari,
5. Cheti cha kuzaliwa,


5. Cheti cha kuzaliwa,
6. Nakala ya kitambulisho cha taifa/mzanzibari,
7. Nakala ya cheti cha usajili kwa mawakili kutoka Tanzania Bara, Kenya, Uganda, Rwanda, Burundi, na nchi nyengine za Jumuiya ya Madola,
8. Cheti cha kuonesha uhai wa uwakili '*current practicing certificate*'
9. Barua ya mdhamini,
10. Uthibitisho wa tabia nzuri ya muombaji.

Sifa zinazohitajika kwa waombaji wa uvakili:

1. Awe na Stashahada ya sheria kutoka katika chuo kikuu au taasisi inayotambuliwa na Serikali
2. Awe amepata mafunzo maalum ya masuala ya sheria kwa kipindi kisichopungua miezi mitatu kutoka katika Skuli ya Sheria ya Zanzibar au yengine kama hiyo inayotambuliwa na Baraza la Mawakili.

Viambatanisho katika maombi ya uvakili:

1. Nakala ya cheti cha stashahada ya sheria,
2. Nakala ya matokeo ya kitaaluma (Transcript),
3. Nakala ya cheti cha mafunzo maalum ya masuala ya sheria kwa mavakili,
4. Nakala ya vyeti vya elimu ya sekondari,
5. Cheti cha kuzaliwa,
6. Nakala ya kitambulisho cha taifa/mzanzibari,
7. Barua ya mdhamini,
8. Uthibitisho wa tabia nzuri ya muombaji.


.....
CHAUSIKU K. KUYA
NAIBU MRAJIS
MAHKAMA YA ZANZIBAR
11/07/2023

